MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 32. Msimu wa kilimo 2016/17 Tathmini ya Kipindi cha Agosti 11-20, 2017 na matazamio kwa kipindi cha Agosti 21-31, 2017**

**MUHTASARI**



- Katika kipindi cha Agosti 11-20, 2017, msimu wa kiangazi uliendelea ijapokuwa mvua nyepesi za nje ya msimu wa mvua zilinyesha katika maeneo machache ya mikoa ya Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu, Manyara, Kilimanjaro, Pwani, Dar es Salaam na kisiwa cha Unguja.
- Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa hazitoshelezi kwa uoteshaji wa mazao hata hivyo zinaweza kuathiri ubora wa mavuno yasiyohifadhiwa vizuri na mazao ambayo hayajavunwa.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasababisha upungufu wa maji kwa mifugo, hivyo wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji na malisho.
- Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2017

Katika kipindi tajwa hapo juu, mifumo ya hali ya hewa katika kizio cha kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika zaidi ilihali mifumo ya hali ya hewa katika kizio cha kaskazini (Azores na Siberia) ilipungua nguvu zaidi. Hali hiyo ilichangia ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kuwa katika kizio cha kaskazini mwa dunia. Joto la bahari kusini mashariki mwa Bahari ya Hindi lilikuwa juu ya wastani, ilihali katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola), lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2017

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa tajwa hapo juu, msimu wa kiangazi uliendelea. Hata hivyo, mvua nyepesi za nje ya msimu wa mvua zilinyesha katika maeneo machache ya mikoa ya Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu, Manyara, Kilimanjaro, Pwani, Dar es Salaam na kisiwa cha Unguja kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.




**Kielelezo 1**. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Agosti 11-20, 2017.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2017

Shughuli za kilimo zimepungua katika maeneo mengi nchini, na wakulima wako katika hatua za awali kujiandaa kwa ajili ya mvua za *vuli* kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua na msimu kwa maeneo ya yanayopata msimu mmoja wa mvua. Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Arusha na Manyara ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua kuliko maeneo mengine nchini.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito na mabwawa viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo inayoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2017

Mifumo ya hali ya hewa katika kizio cha kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika zaidi, ilihali mifumo katika kizio cha kaskazini inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hiyo inatarajiwa kuchangia ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kuwa katika kizio cha kaskazini. Joto la bahari magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea kuwa juu ya wastani ilihali katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola), joto la bahari linatarajiwa kuwa la chini ya wastani. Kutokana na kuongezeka nguvu kwa mifumo ya hali ya hewa katika kizio cha kusini, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2017

Maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu pamoja na vipindi vya baridi. Hata hivyo mvua nyepesi za nje ya msimu zinatarajiwa katika maeneo machache ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu na Shinyanga), nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara), pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba**),** nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Iringa, Songwe na Mbeya), pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na ukanda wa kusini (Mikoa ya Njombe na Ruvuma). Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa hususan katika maeneo ya pwani yaani mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Lindi, Mtwara, Pwani na visiwa vya Unguja and Pemba.

## MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2017

Hali ya ukavu na upepo inayotarajiwa itaathiri upatikanaji wa maji kwa maeneo mengi nchini. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa hazitoshelezi kwa uoteshaji wa mazao ya msimu bali zinaweza kuathiri mavuno yasiyohifadhiwa vizuri na ambayo hayajavunwa. Wafugaji na wakulima kote nchini wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa. Wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki zikiwemo matumizi endelevu ya maji na malisho yaliyopo kwa kuzingatia ushauri kutoka kwa maafisa ugani katika maeneo yao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali inayotarajiwa ya ukavu pamoja na upepo. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Baruapepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz*